

**Jaji >>Alitoa kauli hiyo katika sherehe za k**

UHURU UK 4

## Wafugaji wapewa mbinu za kuboresha mifugo yao

**Kibaha**  
Na SCOLASTICA MSEWA

MENEJA wa shamba la malisho Vikuge liliopo Kongwe Kibaha mkoani Pwani, Ruben Ngailo amewataka wafugaji kulima malisho badala ya mifugo ili kupata mazao bora.

Akizungumza jana katika shamba hilo, alisema mahitaji ya malisho hasa kipindi cha kiangazi ni makubwa ambayo hayatoshelezi soko la ndani ya nchi.

Ngailo alisema baadhi ya magonjwa kuletwa kutokana na mifugo kula chakula kisichokuwa salama hivyo, aliwahimiza wafugaji kulima mashamba ya malisho ili kupata mazao bora.

Pia aliwataka vijana kuchangamkia kilimo cha malisho ya mifugo ili kupata fedha na kuijinua kiuchumi na kujiletea maendeleo.

"Vijana wana wajibu wa kulima mashamba ya kulisha mifugo ili wajipatie kipato na kujenga uchumi wao, hawana sababu ya kulalamika kwamba hawana ajira," alisema.

Ngailo alisema mwaka huu wameongeza ekari za kulima majani ya malisho ya mifugo kutoka 230 mwaka jana hadi 437 mwaka huu katika shamba hilo la Vikuge.

Aidha, meneja huyo alidokeza wameongeza ekari tano za mahindi ambayo yatatumika kwa malisho ya mifugo.



**JAJI** Kiong  
watatu w  
kwa maja  
kwa Jaji K

**Vijana wana  
wajibu wa kulima  
mashamba ya  
kulisha mifugo  
ili wajipatie  
kipato na kujenga  
uchumi wao,  
hawana sababu  
ya kulalamika  
kwamba hawana  
ajira.**

**J  
ku**

NA REHEN

**W**

Hayo  
Mahakama  
jiji Dar es  
Jaji Siya  
za kuwa  
wastaifu  
Mugeta, Be  
Jaji S  
mahakama  
ngumu ku  
na watur  
imanl kwa  
Mahakama  
Katika

**Dar vaiinanga k**

Uhuru


  
MAONI YA MHARIRI



## Wadau washirikishwe utekelezaji vipaumbele Sekta ya Mifugo

JUMANNE wiki hili, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alianika mikakati ya wizara yake katika kutekeleza vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Waziri huyo avitaja baadhi ya vipaumbele hivyo ni kuanzisha skimu za umwagillaji katika mashamba ya malishi ya Vluge na Langwira, na ranchi za NARCO za Kongwa na Mzeri, kujenga mabwawa na visima virefu kwa ajili ya mifugo, kuanzisha mashamba darasa 150 katika mamlaka za serikali za mitaa na taasisi za wizara.

Alitaja kipaumbele kingine ni kuanzisha vituo vipyta ya uwekezaji ya vijana na kuendeleza vituo vingine vilivoanzishwa, kuhimilisha ng'ombe 100,000, kuendelea kununua madume bora na kuyagawa kwenye vikundi ya wafugaji, kununua ng'ombe wazazi 1,200 kwa ajili ya mashamba ya serikali ya kuzalisha mitambua na kuzalisha dozi 1,500,000 za mbegu bora za mifugo katika kituo cha NAIC.

Kingine ni kuendesha kampeni ya udhibiti magonjwa kwa kujenga majosho 246, kununua dawa za kuogesha mifugo lita 56,000 na kusambaza chanjo dozi 500,000,000, kununua pipipiki 1,200 na magari matatu, zana za huduma za veterinari 1,100 na zana za uhimilishaji 184.

Pia, alisema wizara yake itaananza kampasi mpya ya LITA Songwe, kukamilisha taratibu za upatikanaji wa ithibati kwa mbegu za malishi ili ziuzwe madukani na kuanzisha kituo cha utafu wa mifugo cha Kanda ya Magharibi Wilayani Nsimbo mkoza wa Katavi.

Waziri huyo alitaja kipaumbele kingine ni kuanzisha skimu za unenepeshaji katika mashamba ya NARCO na Vituo ya kupumzishia mifugo, kujenga na 54 kukarabati minada, kufunga mizani katika minada 70 ya awali na kujenga vituo 10 ya kukusanya maziwa.

Pia, alisema wizara hiyo itaiwezesha NARCO kuzalisha ndama 5,479 kutokana na majike wazazi 6,849 na kunenepeshia ng'ombe 12,696 kuitia programu ya kujenga uwezo wa uwekezaji kwa vijana itakayofanya katika ranchi ya NARCO Kongwa.

Vilevile, itazalisha marobota ya hei 55,000 katika ranchi ya Kongwa na Mzeri, kukusanya maoni ya wadau na kufanya tathmini ya uanzishaji wa Mamlaka ya Kusimamia na Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na kuvutia wawekezaji katika mbegu bora za kuku, vyakula ya mifugo, dawa, chanjo, uzalishaji wa mbari za mifugo na mbegu za malishi.

Alitaja kipaumbele cha 10 ni kutambua na kusajili katika mfumo wa kielektroniki mifugo milioni 40.6 ili kuwa na taarifa sahihi kwa ajili ya kuboresha mifugo na kukidhi hitaji la masoko.

Tunaimani kwamba utekelezaji wa vipaumbele hivyo ili ufanikiwe kama iliyopangwa ni muhimu wadau wa sekta ya mifugo wakashirikishwa katika utekezaji wa mpango na utoaji maoni II kuondoa sintofahamu inayosababishwa kutoshirikishwa wadau.

Mara nyangi changamoto zinazoitokeza katika utekelezaji mipango inayogusa sekta ya mifugo, chanzo kilikubwa ni ushirikishwaji hafifu kwa wadau hususan wafugaji, hivyo tunaa minni endapo wizara itazingatia ushirikishwaji wadau, mafanikio makubwa yatapatikana.

### Uhuru Publications Limited (UPL)

S.L.P. 2072, Dodoma,

Ofisi Ndogo ya Makao Makuu Dodoma: Mtaa wa Makongoro Area C  
Chumba cha Habari:

+255-784 - 414194, 0784 - 446797

email: uhuruvijijini@gmail.com

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu	0655 355810
Naibu Mhariri Mtendaji:	0784 - 599717

Mhariri Mkuu:	0784 - 414194
---------------	---------------

Mhariri wa Habari:	0784 - 446797
--------------------	---------------

Mhariri wa Michezo:	0718 - 611700
---------------------	---------------

Idara ya Siasa na Habari:	0713 - 363337
---------------------------	---------------

### IDARA YA BIASHARA

Meneja Biashara:	0754 - 313140
Meneja Matangazo:	0765 - 142207
Meneja Uzalishaji na Mauzo:	0784 - 308534

### REDIO UHURU FM (PMCL)

uhurufmnews@gmail.com

Kalmu Mkurugenzi Uhuru FM	0765 - 383757
---------------------------	---------------

Kalmu Mhariri Mkuu Uhuru FM:	0713 - 248640
------------------------------	---------------

Meneja masoko Uhuru FM:	0715 - 584 150
-------------------------	----------------

# \*TAFICO to increase sea fish exports by 30pc

**By BATIVA MINJA**

TANZANIA Fishing Corporation (TAFICO) plans to increase sea fish export by 30 per cent in five years from currently 30,000 tonnes annually.

The Ministry of Livestock and Fisheries Permanent Secretary, Prof Riziki Shemdoe told 'Daily News' yesterday that the initiative comes after securing 2.6bn/- from Japan International Cooperation Agency (JICA).

"With the funds, TA-

FICO will acquire a new 22-metre long fishing vessel with a capacity of 90 tonnes for deep sea fishing," he said.

He said the funds will also be used for the construction of cold storage warehouse and purchase of refrigerated vehicle.

He said TAFICO in its 10-year plan has various projects to be implemented in phases that will boost GDP and create about 20,000 jobs.

Prof Shemdoe said also that the government has set

aside 3.4bn/- in the 2023/24 financial year to revive TAFICO and boost its contribution to economic growth.

He said TAFICO will engage in buying fish from small scale fisheries, add value and sell them to local and foreign markets.

Further, in efforts to address post harvest losses, TAFICO will establish sardine and small pelagic fish processing project to dry about 80 to 100 tonnes of sardines per month.

Statistics show that there

has been up to 40 per cent post-harvest losses of fish during huge harvest.

He said the government future plan is to promote the development of the fishing industry and ensure fishing operations extend to the Tanzanian Exclusive Economic Zone (EEZ) and beyond in order to capitalise on the richness of the deep-sea fishery.

Prof Shemdoe said the government is determined to invest more in order to benefits from deep sea fishing.

**The Ministry of Livestock and Fisheries Permanent Secretary, Prof Riziki Shemdoe told 'Daily News' yesterday that the initiative comes after securing 2.6bn/- from Japan International Cooperation Agency (JICA).**